Enyi mlioamini, muitikieni Allah s.w na Mtume wake anapokuiteni katika yale yatakakupeni uhai......

# Khilafah
## ndio suluhisho

RAMADHAN 1438 A.H. ··· MEI/JUNE 2017··· TOLEO: 58




# VIBARAKA NI KIKWAZO KWA UISLAM

YALIYOMO:

1. KARIBU MTUKUFU RAMADHANI
2. ISTILLAH AHLUSUNNAH
3. KUYAKIMBIA MAASI KATIKA RAMADHANI
4.SWALI KWA AMIR: ZAKAT YA FAIDA YA BIASHARA
5. SAUDIA: CHAGUO LA KWANZA LA TRUMP


jkhilafahtz@gmail.com

DONDOO ZA HABARI

## // TRUMP NA HADAA ZA KIMFUMO

Raisi wa Marekani Donald Trump ameendelea kudhihirisha uchanga wake wa siasa hasa za kimfumo na kimataifa baada ya kupuuzia kuongelea kipengele cha tano (Article 5) cha mkataba wa NATO kwa namna Marekani itakavyo tekeleza.

Raisi huyu wa 45 alitegemewa atoe ahadi ya kuisaidia NATO ikitokea nchi yoyote ndani ya umoja huo itashambuliwa. Kipengele



hicho kinatoa msisitizo kuwa akishambuliwa mwanachama yeyote wa NATO itamaanisha wameshambuliwa wanachama wote. Hajawahi Raisi yeyote wa Marekani kuhoji kipengele hicho kabla ya Trump.

Kifungu hiki kilianzishwa kufuatia shambulio lililoitwa la 'kigaid' la septemba 11. Ikiwa ni mkakati wa pamoja kuunda nguvu ya kupambana na kila shambulio na washambuliaji. Nikifungu kinacho imarisha mashambulizi kwa kila atakaye vikwa sifa ya ugaidi, ima mtu binafsi, kikundi au nchi. Kwahiyo ni katika mikakati ya sera za kinje.

Hali hii inatilia mkazo jawabu lake alipo hojiwa na New York Times interview 1 July ya mwaka uliopita , kuwa yuko tayari kuzilinda dola ndogo ikiwa zitavamiwa na Urusi , akajibu kuwa atafanya hivyo kwa sharti zitalipa na namnukuu,"ikiwa watatimiza sharti hilo ,ndio tutazilinda."

## // SAUDIA YA TUMIA ZAIDI YA DOLA MILIONI 68 ZIARA YA TRUMP

Saudi Arabia imetumia zaidi ya Dola milioni 68 katika mapokezi ya Rais wa Marekani,



Donald Trump. Mfalme Salman wan nchi hiyo alimuandikia waziri wa fedha kuhusu kutengwa kwa Rial milioni 257 (Takriban dola milioni 68). Fedha hizi ni kwa ajili ya burudani na gharama za mkutano ulio jumuisha warabu na waamerika. http://alwaght.com/en/News/96742/Saudi-Arabia-Spending-$68-Million-to-Host-Donald-Trump

Gharama hizi ni nje ya takriban dola bilioni 110 zilizo tumika kununulia silaha kutoka kwa Marekani, silaha ambazo kwa namna ilivyo Saudia zitatumika kuzidi kuwaua waislam wa nchi jirani kama Yemen kwa maelekezo ya mabwana zake. Kwani silaha hizo zimelenga kusaidia washirika na jeshi la marekani katika ghuba ya uajemi. http://www.foxnews.com/politics/2017/05/20/trump-arrives-to-saudi-arabia-for-his-first-international-trip-since-taking-office.html

## // Mripuko wa Manchester: JINAMIZI LA UGAIDI KWA WAMAGHARIB

Mauaji ya zaidi ya watu 22 yaliyotokea baada ya mlipuko jijini Manchester



Uingereza ni dalili wazi za hadaa za wamagharibi kwa ummah. Ametajwa Salman Abeid, mualgeria kuhusika. Eti bado polisi ina shaka na hofu na inahaha kutafuta wahusika ikiamini wapo wengi nyuma ya mlipuaji.

Lakini swali la kushangaza nivipi nchi kama hizi zinazojinadi kuendelea kiulinzi na usalama ziwe rahisi kushambuliwa na iwe tabu kuwabaini wahusika.

Bilashaka ni kuimarisha kampeni ya ugaidi ili kufikia malengoyao katika kupambana na uislam na waislam duniani.

## // USANII WA KUCHELEWA KUSAINI MKATABA WA EPA:

Mara tu baada ya kupokea kijiti cha uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museven, ameweka wazi msimamo wa Jumuiya hiyo kutokusaini mkataba huo. EPA ni Mkataba wa Ushirikiano wa Kibiashara baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Nchi za Umoja wa Ulaya (EU).



Tanzania na Uganda ndiwo wamekataa kuusaini mkataba huo wakiutazama kama ukoloni mamboleo. "Tutawezaje kujadili na kusaini mkataba hali ya kuwa mwanachama wetu mmoja amewekewa vikwazo na EU ? bado tunahitaji ufafanuzi juu ya mambo kadhaa yaliyomo kwenye mkataba wa EPA," alisema Museveni. Aliongeza kwamba ataongoza ujumbe maalumkwenda makao makuu ya EU kubainisha msimamo wao huo.

Msimamo huu ni kama kiini macho kwani nchi hizi, hasa Uganda imo katika mashirikiano yasiyo na tija kwa taifa lake, suala la Somalia na ugaidi. Uganda imekuwa mstari wa mbele kutumia jeshi lake kwa mwamvuli wa jeshi la Afrika hukumamia ya askari hao wakiangamia na rai wakiishi kwa mashaka bila amani wakihofia muda wowote kushambuliwa na walipa kisasi.
Japo la msingi ilikuwa kuonesha msimamo katika kutumiwa huku na sio katika EPA ambayo mwishowe lazima watasaini.

# Tahariri

# MTUKUFU RAMADHANI TUNAKUPOKEA KWA FURAHA NA MAJONZI

Allah SWT anasema : شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَى مَا هَدَاكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

*Mwezi huo mlioambiwa mfunge ) ni mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa Qurani ili iwe ni uongozi kwa watu, na hoja zilizowazi wa uongozi na upambanifu wa haki na batili.Atakayekuwa katika mji ndani ya mwezi huu afunge.Na mwenyekuwa mgonjwa au safarini ,basi na atimize hisabu ya siku alizoacha kufunga katika siku nyengine.Allah SWT anakutakieni yaliyo mepesi na wala hakutakieni yaliyo mazito.na pia anakutakeni kumtukuza Yeye kwa kuwa amekuongozeni ili mpate kushukuru.*

Aya imeeleza wazi juu ya utukufu wa Mwezi wa Ramadhani , na mwenye kufunga vile inavyotakiwa ana ujira mkubwa .Shime waislamu sote tufanye ibada hii ikiambatana na ibada nyengine za kusoma Qurani,kukirimu masikini na mafukara,kufuturishana miongoni mwetu , kutoa sadaka , kusoma Qurani kwa wingi , ibada za tarawehe na nafila mbali mbali za usiku, tutembelee wagonjwa na kila lenye kheri na haki ili tupate radhi ya Mola wetu.

Hayo kwa upande wa kiroho, lakini aya pia imetueleza Qurani ni uongozi kwa watu ikitubainishia kuwa sisi wanadamu hatutakiwi tuchukuwe uongozi wa aina yoyote uliotengenezwa na mwanadamu zaidi ya ule wa Allah SWT.Kwa ufafanuzi huu ni makosa makubwa kwa mwanadamu yo yote kuchukuwa na kuifanyia kazi mifumo hii ya ubepari/demokrasia ambayo imetengenezwa na mwanadamu.

Makafiri asli yao ni kupinga kila fikra na njia alotuletea Allah SWT. Haja yao ni kuishi maisha watakayo hapa duniani wafanye kila ufisadi katika ardhi. Kuanzia kumwaga damu ovyo, kukithiri kwa uchafu ,maovu na zinaa , kudhulumu wanyonge na kuwatesa na kuwazidishia umasikini, kuzipora mali katika nchi kadhaa za kiislamu kupitia vibaraka waliowaweka katika nchi hizo na kujenga viwanda vikubwa vya kutengenezea silaha kali ili kila aliyezinduka asithubutu kuwaondoa katika uhondo wao hapa ulimwenguni.Haja ya pili ni kuwapotoa watu wengi ili wasipate adhabu ya Allah peke yao.Ndiyo maana wakaleta mfumo wao wa demokrasia na kuufunika pazia watu waukumbatie na kuufuata bila kujuwa kuwa ni ukafiri wa wazi.

Makafiri wakiongozwa na Marekani wakabuni mbinu nyengine mbaya zaidi ya kuzitawala nchi za kiislamu kupitia vibaraka wao na kuhakikisha waislamu hawapati mwamko wa kurejea katika Qurani kama mwongozo wao bali wajaze fikra za ukafiri katika mabongo yao na wapotoke kama walivyopotoka wao.Na ndio maana vinaundwa vita visivyo na mashiko katika ardhi za waislamu kumwaga damu zao na kuivunja miji yao huku wakiongeza umasikini kwao.Wakatengeneza pia msamiati wa uadui wa ugaidi na uislamu wa siasa kali. Si ajabu kuona Saudia na vibaraka wengine kusaidia kwa hali na mali kuivamia Yemen,Misri kuangamiza halaiki ya waislamu, palestina kuwekwa rehani na kuiangamiza, Afghanistan, Somalia, Syria na kwengineko. Si ajabu kuona makafiri wameingiza mizozo na ikhtilafu ya madhhebu baina ya mashekhe ambayo haina umuhimu wowote mbele ya Allah SWT bali ni kuwapa nguvu maadui wa Allah.

Enyi waislamu wenzangu , Tuitumie Ramadhani , huku tukirejea Qurani , na kutafakari vipi itafanyakazi iwe mwongozo kwetu kivitendo. Mtume saaw ametuonyesha njia ya kutekeleza mwongozo wa Qurani kivitendo kwa kuanzisha dola ya kiislam Madina na Maswahaba wakafata nyayo zake ,sasa dola hiyo haipo.Ni wajibu wetu sote kufanyakazi kidaawah kuirejesha ili Qurani irejee kuwa mwongozo wetu katika maisha yetu.

**MHARIRI**

**JARIDA LA KHILAFAH**

**Ramadhani 1438**

# ISTILAHI YA "AHLUSUNNAH WALJAMAA"

**Sehemu ya Nne**

## HISTORIA YA AHLUSUNNA WALJAMA'A

**Na: Abu Malik Thair Salama**

Kwanza : Istilahi ya "Alajmaa" ina Maana maalum ya Kisheria .

Limepokelewa katika hadithi nyingi za Mtume ( S.a.w ) Tamko la "Aljamaa" likiongezewa Mbele yake neno "Almuslimiina" na Miongoni mwa Hizo :

نَضَّرَ اللَّهُ »، قال: rعن أنس بن مالك رضي الله عنه أن رسول الله
عَبْدًا سَمِعَ مَقَالَتِي هَذِهِ فَحَمَلَهَا، فَرُبَّ حَامِلِ الْفِقْهِ فِيهِ غَيْرُ فَقِيهٍ،
وَرُبَّ حَامِلِ الْفِقْهِ إِلَى مَنْ هُوَ أَفْقَهُ مِنْهُ، ثَلَاثٌ لَا يُغِلُّ عَلَيْهِنَّ صَدْرُ
مُسْلِمٍ: إِخْلَاصُ الْعَمَلِ لِلَّهِ، وَمُنَاصَحَةُ أُولِي الْأَمْرِ، وَلُزُومُ جَمَاعَةِ
، رواه أحمد وابن « المسلمين، فَإِنَّ دَعْوَتَهُمْ تُحِيطُ مِنْ وَرَائِهِمْ
ماجه وهو حديث حسن،

( Toka kwa Anas Bin Malik ( R.a ) kwamba Mtume ( S.a.w ) amesema : Allah aung'arishe uso wa Mja ambaye amesikia maneno yangu haya na akayabeba ( Akayachukuwa ) basi huenda aliebeba Fiqhi(Ujuzi ) sio mjuzi katika hilo,na huenda aliyebeba Ujuzi akamfikishia Yule ambaye ni Mjuzi kuliko yeye,Mambo Matatu Kila moyo wa Muislam ni lazima Usichukie ukweli wa kufanyia kazi, Kufanya amali kwa Ikhalas kwa ajili ya Allah,na kuwapa nasaha viongozi,na kujilazimisha kuwa pamoja (Kushikamana na Jamaa (Kundi ) ya Waislam....)Kaipokea Imam Ahmad na Ibn Maajah na ni Hadithi  Hasan.

قَامَ فِينَا رَسُولُ اللَّهِ » خطب عمر رضي الله عنه بالشام فقال:
مَقَامِي فِيكُمْ، فَقَالَ: اسْتَوْصُوا بِأَصْحَابِي خَيْرًا، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ، r
ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ، ثُمَّ يَفْشُو الْكَذِبُ حَتَّى يُعَجِّلَ الرَّجُلُ بِالشَّهَادَةِ
قَبْلَ أَنْ يُسْأَلَهَا، وَبِالْيَمِينِ قَبْلَ أَنْ يُسْأَلَهَا، فَمَنْ أَرَادَ بُحْبُوحَةَ الْجَنَّةِ
فَلْيَلْزَمِ الْجَمَاعَةَ، فَإِنَّ الشَّيْطَانَ مَعَ الْوَاحِدِ، وَمِنَ الاثْنَيْنِ أَبْعَدُ،
رواه الترمذي «فَمَنْ سَرَّتْهُ حَسَنَتُهُ وَسَاءَتْهُ سَيِّئَتُهُ فَهُوَ مُؤْمِنٌ
وأحمد، وهو حسن صحيح،

Alihutubu Khalifah Omar ( R.a ) akiwa Sham,akasema : Alisimama Mbele yetu Mtume ( S.a.w) kama nilivyosimama Mbele yenu,akasema : Nakuusieni kuwaanyia kheri Maswahaba zangu,kisha watakaowafuana,kisha watakaowafuata,kisha utaenea uongo,kiasi kwamba mtu atafanya haraka kutoa Ushahidi kabla hajaambiwa atoe ushahidi,na ataapa kabla hajaambiwa aape,Basi mwenye kutaka ( Katikati ) Neema za peponi basi awe pamoja na Jamaa,kwani Shetani huwa na Mtu mmoja,lakini kwa watu wawili anakuwa mbali,basi Yule ambaye atafurahishwa na mema yake na kuchukizwa na maou yake basi huyo ni Muumini.) Kaipokea Imam Ahmad na Ibn Maajah na ni Hadithi  Hasan.

( قال: فما معنى أمر النبي بلزوم جماعتهم؟ قلت: لا معنى له إلا
واحد. قال: فكيف لا يحتمل إلا واحداً؟ قلت: إذا كانت
جماعتهم متفرقة في البلدان فلا يقدر أحد أن يلزم جماعة أبدان
قوم متفرقين، وقد وجدت الأبدان تكون مجتمعة من
المسلمين والكافرين والأتقياء والفجّار، فلم يكن في لزوم
الأبدان معنى، لأنه لا يمكن، ولأن اجتماع الأبدان لا يصنع
شيئاً، فلم يكن للزوم جماعتهم معنى، إلا ما عليه جماعتهم
من التحليل والتحريم والطاعة فيهما. ومن قال بما تقول به
جماعة المسلمين فقد لزم جماعتهم، ومن خالف ما تقول به
جماعة المسلمين فقد خالف جماعتهم التي أمر بلزومها)

Katika hadithi hizi mbili kuna amri ya wazi ya kuwa pamoja na Jamaa ya Waislam,na nimevutika na maneno Mazuri  ya Imam Shafii Allah amrehemu akibainisha katika maneno hayo maana ya Amri ya Mtume ( S.a.w) ya kuwa pamoja na Jamaa ya Waislam,baada ya Imam Shafii kutaja Hadithi ya Omar iliopita akasema (Ni maana ya Amri ya Mtume ( S.a.w ) kujilazimisha kuwa na Jamaa? Nimesema : Haina maana isipokuwa Moja.akasema : Ni vipi isiwe na zaidi ya maana moja ? Nimesema : Pindi Ikiwa Jamaa yao imetawanyika katika Miji,hatoweza Mtu yeyote ajilazimishe kuwa kwenye Jamaa ya watu tofauti waliotawanyika,na ukikuta watu wamekusanyika baina yao kuna waislam,Makafiri,Wachamungu na Waovu,inakuwa haina maana ya kukusanyika kwa miili yao,kwa sa-

# AHLUSUNNAH...

...*INATOKA UK 4*

Na zingatia Jambo la tatu Muhimu : Kukusanyika kwa Miili hakutengenezi Jamaa,na wala hakuna maana yeyote,isipokuwa kile ambacho kinaunda Jamaa ambayo Muislam analazimika awe nayo na asitoke humo ni Jamaa yaani kukusanyika kwao katika Ufahamu,na Ufahamu au Fikra ndio msingi wa kuitambulisha Jamii na kuitofautisha na maana ya Jamaa,Imam Shafii ( Rahimahullah ) anatofautisha tofauti ya kina baina ya Mkusanyiko wa watu na Baina ya Jamii.

عن حذيفة بن اليمان رضي الله عنه قال: كَانَ النَّاسُ يَسْأَلُونَ
عَنِ الخَيْرِ، وَكُنْتُ أَسْأَلُهُ عَنِ الشَّرِّ، مَخَافَةَ أَنْ rرَسُولَ اللَّهِ
يُدْرِكَنِي، فَقُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، إِنَّا كُنَّا فِي جَاهِلِيَّةٍ وَشَرٍّ، فَجَاءَنَا
«نَعَمْ» اللَّهُ بِهَذَا الخَيْرِ، فَهَلْ بَعْدَ هَذَا الخَيْرِ مِنْ شَرٍّ؟ قَالَ:
«نَعَمْ، وَفِيهِ دَخَنٌ» قُلْتُ: وَهَلْ بَعْدَ ذَلِكَ الشَّرِّ مِنْ خَيْرٍ؟ قَالَ:
قَوْمٌ يَهْدُونَ بِغَيْرِ هَدْيِي، تَعْرِفُ مِنْهُمْ »قُلْتُ: وَمَا دَخَنُهُ؟ قَالَ:
نَعَمْ، دُعَاةٌ »وَتُنْكِرُ قُلْتُ: فَهَلْ بَعْدَ ذَلِكَ الخَيْرِ مِنْ شَرٍّ؟ قَالَ:
قُلْتُ: يَا رَسُولَ «عَلَى أَبْوَابِ جَهَنَّمَ، مَنْ أَجَابَهُمْ إِلَيْهَا قَذَفُوهُ فِيهَا
«هُمْ مِنْ جِلْدَتِنَا، وَيَتَكَلَّمُونَ بِأَلْسِنَتِنَا» اللَّهِ صِفْهُمْ لَنَا، قَالَ:
تَلْزَمُ جَمَاعَةَ »قُلْتُ: فَمَا تَأْمُرُنِي إِنْ أَدْرَكَنِي ذَلِكَ؟ قَالَ:
قُلْتُ: فَإِنْ لَمْ يَكُنْ لَهُمْ جَمَاعَةٌ وَلاَ إِمَامٌ؟ «المُسْلِمِينَ وَإِمَامَهُمْ
فَاعْتَزِلْ تِلْكَ الفِرَقَ كُلَّهَا، وَلَوْ أَنْ تَعَضَّ بِأَصْلِ شَجَرَةٍ، حَتَّى »قَالَ:
رواه البخاري ومسلم «يُدْرِكَكَ المَوْتُ وَأَنْتَ عَلَى ذَلِكَ

Kutoka kwa Hudheifah Bin Al-yamaan ( R.a ) amesema : al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Hudhaydah bin al-Yamaan (Radhiya Allaahu ´anh) ameleezea kuwa watu walikuwa wakimuuliza Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) juu ya kheri ambapo mimi namuuliza juu ya shari kwa kuchelea nisije kutumbukia ndani yake. Nikasema: "Ee Mtume wa Allaah! Sisi tulikuwa katika Jaahiliyyah na shari ambapo Allaah akatuletea kheri hii. Je, baada ya kheri hii kuna shari?" Akasema: "Ndio." Nikasema: "Je, baada ya shari hiyo kuna kheri?" Akasema: "Ndio, na itakuwa na moshi." Nikasema: "Ni watu wanatokamana na ngozi yetu na wanazungumza lugha kama yetu." Nikasema: "Unaniamrisha nini pindi nitapokutana na hilo?" Akasema: "Jilazimie na mkusanyiko wa waislamu na kiongozi wao." Nikasema: "Ikiwa hawana mkusanyiko wala kiongozi?" Akasema: "Jitenge na hayo mapote yote hata kama utahitajia kuuma mashina ya mti mpaka mauti yakukute na wewe uko katika hali hiyo."

Tusifie nao." Akasema: "Ni watu wanatokamana na ngozi yetu na wanazungumza lugha kama yetu."

Zingatia hapa : “Pasina kuwepo Jamaa ya Waislam na Kiongozi wao” ni maelezo ya kubainisha Vikundi ambavyo ni wajibu kujitenga navyo.na ni wajibu kuwa pamoja na Jamaa na Imam,Haiwezi kuwepo Jamaa pasina Imam,kwa sababu kama ingeweza kupatikana pasina Imam/Kiongozi basi ingewezeka  kushikamana na hiyo Jamaa wakati wa kutokuwepo kiongozi,kwa hiyo haiwezekani kuwepo Imam yaani Khalifah isipokuwa awe ni khalifah kwa Jamaa wa Waislam.!

عن الحارث الأشعري رضي الله عنه قال: قال رسول الله r:
فذكر «إِنَّ اللَّهَ أَمَرَ يَحْيَى بْنَ زَكَرِيَّا بِخَمْسِ كَلِمَاتٍ...»
وَأَنَا آمُرُكُمْ بِخَمْسِ كَلِمَاتٍ » :rالحديث بطوله، قال رسول الله
أَمَرَنِي اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ بِهِنَّ: الْجَمَاعَةُ، وَالسَّمْعُ وَالطَّاعَةُ، وَالْهِجْرَةُ،
وَالْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، فَمَنْ خَرَجَ مِنَ الْجَمَاعَةِ قِيدَ شِبْرٍ فَقَدْ
رواه الترمذي وأحمد، «خَلَعَ رِبْقَةَ الْإِسْلَامِ مِنْ عُنُقِهِ إِلَّا أَنْ يَرْجِعَ

Kutoka kwa Alhaarith Al-Ash’ariy ( R.a ) amesema :Amesema Mtume ( S.a.w ) : Hakika Allah amemuamrisha Zakaria Bin Yahya kwa Maneno Matano.......akaitaja Hadithi kwa Urefu wake,amesema Mtume ( S.a.w ) : Namimi Nakuamrisheni Maneno Matano,ameniamrisha kwa hayo Mola wangu Mtukufu,Jamaa,na kusikia na kutii,na kuhama na Jihadi katika Njia ya Allah,Basi yeyote mwenye kutoka katika Jamaa kwa kiasi cha Shibri moja kwa hakika amevua fundo ya Uislam shingoni mwake isipokuwa arejee tena katika Uislam) ameipokea Tirmidhii na Ahmad.

Toka kwa Ibn Abbas amesema :Toka kwa Mtume (S.a.w )

مَنْ كَرِهَ مِنْ أَمِيرِهِ شَيْئًا »قال: rعن ابن عباس عن النبي
«فَلْيَصْبِرْ، فَإِنَّهُ مَنْ خَرَجَ مِنَ السُّلْطَانِ شِبْرًا مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً
رواه البخاري،

“ Mwenye kuchukia kwa Kiongozi wake kitu chochote kile basi na asubiri,kwa kumchukiza basi na asubiri,kwani hakuna yoyote yule atakaetengana na Jamaa kwa Shibri moja basi akafa katika hali hiyo,isipokuwa atakuwa amekufa kifo cha Kijahilia”Bukhari

وأخرج الترمذي وابن خزيمة وابن حبان ومصححا من حديث
مَنْ » الحارث بن الحارث الأشعري في أثناء حديث طويل،
«فَارَقَ الْجَمَاعَةَ شِبْراً، فَكَأَنَّما خَلَعَ رِبْقَةَ الإِسْلامِ مِنْ عُنُقِهِ.

Na amepokea Tirmidhi na Ibn Maajah na Ibn Hibban ikiwa ni hadithi sahihi toka kwa Alhaarithi bin Alhaarith Al-ash’ariy katika hadithi ndefu, “ yoyote yule atakaetengana na Jamaa kwa Shibri moja,basi kana kwamba kavua fundo ya UISLAM Shingoni mwake”

NB:Angalia kwa umakini matamko ya Hadithi yanachanganya kati ya kutoka kwenye Jamaa na Kutoka kwa Kiongozi,na hivyo ni kitu kimoja,Kiongozi katika Uislam ni wa Ummah,unampa Ba’ia ya kuwa Khalifah ili awe Mtawala yaani mwenye kusimamia Mambo kwa Mujibu wa Hukumu za Kiislaam,kwa hiyo imekuwa ni jambo la kawaida kuwa kutoka dhidi ya kiongozi ndiko kutoka kwenye Jamaa.

Na vile vile haina maana kutoka kwenye Jamaa kwa kutoka kwa Mwili,Bali ni kutoka kwa Maadili na Ufahamu(Fikra ) ambazo zipo kwenye Jamaa.

وفي الحديث المرفوع: سَمِعْتُ ابْنَ عَبَّاسٍ، يَرْوِيهِ عَنِ النَّبِيِّ
مَنْ رَأَى مِنْ أميره شَيْئًا يَكْرَهُهُ فَلْيَصْبِرْ، فَإِنَّهُ لَيْسَ »، قَالَ: r
عَنِ «أَحَدٌ يُفَارِقُ الْجَمَاعَةَ شِبْرًا فَيَمُوتُ إلا مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً

# Kuyakimbia Maasi katika Ramadhami




Dini ya Kiislaam imeandaa utaratibu bora na mzuri wa kumsimamia Mwanaadamu katika kila sekta ya Maisha yake,na wala Mwanaadamu hakupewa nafasi ya kubuni namna ya kuendesha Maisha haya Mafupi ya Duniani.

Mwanaadamu kaumbwa kwa lengo maalum na ameletwa hapa duniani ili atekeleze maagizo ya Mola wake,na katika kuyafikia hayo ndio maana Uislam umejengewa juu ya nguzo tano ambazo anapaswa Muislamu kuzitekeleza,na miongoni mwa nguzo hizo tano ni Funga ya Ramadhani. Na msingi wake mkubwa ni kumfanya Mwanaadamu awe Mcha Mungu.

Kwa hiyo Funga ni ibada maalum iliyo muhimu sana katika kumuandaa mja kuwa mcha Mungu kwa kule kukataa kwake matamanio ya kimwili. Hivyo Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kwa ukarimu wake ameahidi malipo makubwa kwa wenye kutekeleza ibada hii ili iwe motisha kwao ya kuwawezesha kutekeleza ibada hii kwa hima kubwa na kwa ukamilifu unaotakikana kama tunavyojifunza katika Hadiyth zifuatazo:

Abu Hurayrah ameeleza kuwa Mtume wa Allaah amesema:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : " مَنْ صَامَ رَمَضَانَ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ " رواه البخاري 38 ومسلم 760.

"Mwenye kufunga Ramadhaan akiwa na imani na akawa na matumaini ya kupata malipo kutoka kwa Allaah dhambi zake zote zilizopita husamehewa,

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ : " مَنْ قَامَ رَمَضَانَ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ " رواه البخاري 37 ومسلم 759 . الحديث دليل على فضل قيام رمضان

Na mwenye kusimama kwa Swalah katika mwezi wa Ramadhaan akiwa na imani na matumaini ya kupata malipo (kutoka kwa Allaah), dhambi zake zote zilizopita zitasamehewa. (Al-Bukhaariy na Muslim). Pia Abu Hurayrah ameeleza kuwa Mtume wa Allaah amesema:

يقول الله عز وجل فيما يرويه عنه رسوله ﷺ في الحديث القدسي:

((عن أبي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ يَقُولُ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ اللَّهُ كُلُّ عَمَلِ ابْنِ آدَمَ لَهُ إِلَّا الصِّيَامَ فَإِنَّهُ لِي وَأَنَا أَجْزِي بِهِ وَالصِّيَامُ جُنَّةٌ وَإِذَا كَانَ يَوْمُ صَوْمِ أَحَدِكُمْ فَلَا يَرْفُثْ وَلَا يَصْخَبْ فَإِنْ سَابَّهُ أَحَدٌ أَوْ قَاتَلَهُ فَلْيَقُلْ إِنِّي امْرُؤٌ صَائِمٌ وَالَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ لَخُلُوفُ فَمِ الصَّائِمِ أَطْيَبُ عِنْدَ اللَّهِ مِنْ رِيحِ الْمِسْكِ لِلصَّائِمِ فَرْحَتَانِ يَفْرَحُهُمَا إِذَا أَفْطَرَ فَرِحَ وَإِذَا لَقِيَ رَبَّهُ فَرِحَ بِصَوْمِهِ))

[ متفق عليه]

"Kila amali njema anayoifanya mwanaadamu italipwa mara kumi (Al-Qur-aan 6:160) mpaka kufikia mara mia saba (Al-Qur-aan 2:261). Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amesema: Ila kufunga kwa sababu funga ni kwa ajili Yangu, na ni mimi mwenyewe nitakayeilipa. Mwenye kufunga anakata matamanio yake ya kimwili na anaacha chakula kwa ajili yangu. Kwa mwenye kufunga kuna furaha mbili, furaha moja anaipata wakati wa kufuturu na nyingine wakati atakapokutana na Mola wake. Na hakika harufu ya mdomo wa mwenye kufunga ni bora mbele ya Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kuliko harufu ya miski. Na funga ni ngao. Kwa hiyo atakayefunga miongoni mwenu hataongea maneno ya upuuzi wala hatagombana. Kama itatokea achokozwe na yeyote, au mtu atakakupigana naye, na aseme: Nimefunga." (Al-Bukhaariy na Muslim).

Katika Uislamu kufunga (Swawm) ni kujizuilia kula, kunywa, kuvuta sigara, kuingiza kitu chochote katika matundu mengine mawili kama vile pua na masikio, kujizuia na kujamii, kujitoa manii kwa makusudi au kwa matamanio na kujizuia kujitapisha,

# KUYAKIMBIA MAASI...

...*INATOKA UK 6*

Kufunga kwa maana ya ndani ni pamoja kujizuilia kutenda maovu yote yaliyokatazwa na Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala). Ili Swawm ya mfungaji iwe na maana na yenye kufikia lengo, hana budi kukizuilia (kukifungisha) kila kiungo chake cha mwili - macho, ulimi, masikio, mikono na miguu- pamoja na fikra na hisia zake na matendo aliyokataza Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala).
Funga inamfundisha Mfungaji ayachunge macho yake kwa kujizuilia na kuangalia aliyoyakataza Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala); na pia auchunge ulimi wake kwa kujizuilia na mazungumzo yote aliyoyakataza Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) kama vile kusengenya, kusema uwongo, kugombana na kadhalika, na ayachunge masikio yake kwa kujizuia kufanya yale yote aliyoyaharamisha Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala);na kui funga miguu yake kwa kujizuilia na kuendea yale yote aliyoyakataza Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) na vile vile adhibiti fikra na hisia zake kwa kujizuia na fikra na dhana mbaya ambazo zinampelekea kuvunja amri na makatazo ya Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala). Ni katika maana hii Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anasema katika Hadithi ifuatayo:

Abu Hurayrah amesimulia kuwa Mtume wa Allaah amesema:

فعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : ( مَنْ لَمْ يَدَعْ قَوْلَ الزُّورِ وَالْعَمَلَ بِهِ فَلَيْسَ لِلَّهِ حَاجَةٌ فِي أَنْ يَدَعَ طَعَامَهُ وَشَرَابَهُ ) رواه البخاري

"Yule ambaye haachi kusema uwongo na haachi kufanya vitendo viovu, Allaah hana haja na kuona kuwa anaacha chakula chake na kinywaji chake (yaani Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) hana haja na funga yake." (Al-Bukhaariy).

Anasema Allaah (Subhaanahu wa Ta'alaa):

أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ

ukawarefukia muda, kisha zikawa ngumu nyoyo zao?

Na wengi miongoni mwao ni mafasiki. (Al-Hadiyd: 16)

Ramadhaan imetufikia! Umefika wakati kwa wale waliozama katika shirki, ulevi, (kila aina ya) madhambi na bid'ah, kujirekebisha na kujitakasa kwa Tawhiyd, utiifu kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta'aalaa) na kufuata Sunnah ya Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). Kwa hiyo: Tujirekebishe kuanzia sasa ili kutakasa, nyoyo na viungo vyetu viwe vinamwabudu Allaah (Subhaanahu wa Ta'alaa) Pekee bila ya kumshirikisha.
Tujirekebishe sasa ili kutakasa, viungo vyetu vitende amali zenye kumridhisha Allaah!
Tujirekebishe sasa kisawa sawa, vitendo vyetu viendane sawa na vile atakavyo mola wetu.

Ndugu Waislam tuzidishe wema na tuyakimbie maasi na mabaya yote kwani Matokeo yake basi ni kwamba mwezi utakapomalizika utakuwa bado una athari za maovu. Anasema Allaah (Subhaanahu wa Ta'alaa):

وَاتَّقُوا يَوْمًا تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ تُوَفَّى كُلُّ نَفْسٍ مَا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

Na iogopeni Siku mtayorejeshwa humo kwa Allaah, kisha kila nafsi italipwa kamilifu iliyoyachuma nao hawatodhulumiwa. (Al-Baqarah: 281)
Na Anasema pia:

وَأَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوَى فَإِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ الْمَأْوَى

Ama yule aliyekhofu kisimamo cha Mola wake, na akaikataza nafsi yake na matamanio. Basi hakika Jannah (itakuwa) ndio mahali pake pa kukimbilia. (An-Naziaat: 41)
Na Anasema pia:

أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ وَلَا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَاسِقُونَ

Je, haujafika wakati kwa walioamini kwamba zinyenyekee nyoyo zao kwa dhikri[2] ya Allaah na (kwa) yale yaliyoteremka ya haki, na wala wasiwe kama wale waliopewa Kitabu kabla, ukawarefukia muda, kisha zikawa ngumu nyoyo zao? Na wengi miongoni mwao ni mafasiki. (Al-Hadiyd: 16)

Tunamuomba Allaah (Subhaanahu wa Ta'alaa) Atuongoze sote na ndimi zetu
Ndugu yetu Muislamu! Anza haraka kujitakasa ili moyo wako na viungo vyako viweze kukubali kwa sahali kutekeleza kheri nyingi. Hivi ndivyo mtu anavyojitayarisha kikweli na ndipo atakapofaidika na mwezi mtukufu wa Ramadhaan. Na haya yote uendelea nayo baada ya Ramadhani.

**NA: SHEIKH MUSSA KILEO**

## BAADHI YAMATUKIO MUNASABA NA RAMADHANI

1. Kupewa utume Mtume (SAAW) tarehe 18 Ramadhani kabla ya Hijra.
2. Kufariki Abuu Talib na mama wa waumini Bikhadija kabla ya Hijra
3. Ushindi wa vita vya badri tarehe 17 Ramadhani mwaka 2 Hijria.
4. Ghazwa ya Bani Salim, tarehe 28 Ramadhani mwaka 2 Hijiria
5. Matayarisho ya vita vya Ahzab mwaka wa 5 Hijria
6. Fat-hi Makka, tarehe 10 Ramadhani mwaka 8 Hijria
7. Kuanza kwa vita vya tabuk, mwaka wa 9 Hijria
8. Kuslimu kwa msafara wa Ghuttam mwaka 10 Hijria
9. Kufariki Abdalla bin Omar al Khataabi (ra) mwaka 37 Hijria
10. Kuuwawa kwa Khalifa wa nne Ali bin Abi Talib(ra), mwaka 40 Hijria
11. Fat-h ya Spain(Undalusia) chini ya Tariq bin ziyad (mwaka wa 93Hijria.
12. Kujegwa kwa Azhar(mwaka wa 361. Hijria.

Vita vya Marekani ndani ya Afgha

1



# KUITOLEA ZAKA FAIDA ILIYOPATIKANA

## JIBU LA: AMIR WA HIZB UT TAHRIR

**Swali:**

Assalamu Alaikum, Nina swali kuhusiana na Zakat. Kwanza nianze kwa kukuelea hali ilivyo. Huwa nina pata faida kwa kuuza nyumba. Kwamfano, ninanunua nyumba kwa dola 30, 000 na ninaiuzwa kwa dola 35,000 na hivyo basi baada ya mwaka mmoja nimepata dola 20,000 kama faida. Mwaka uliopita nilikuwa na dola 100,000 na mwaka huu nina dola 120,000. Je, nina wajibika kutoa Zakat katika fungu lipi? Ni katika dola 120, 000 au katika Dola 20,000?.

**Jawabu**:

*Wa Alaikum Assalam wa Rahmatullahi wa Barakatuh,*

Kwa mujibu wa swali lako ni wazi kwamba unafanya biashara ya kununua na kuuza nyumba. Hivyo basi suala la Zakat hapa linakuwa katika msingi wa Zakat ya biashara, na hawaja tofautiana maswahab ra kwamba mfanyabiashara anawajibika kulipa Zakat.

Ana tufahamisha Abu Daud kutoka kwa Samurah bin Jundub aliyesema:

«أما بعد، فإن رسول الله ﷺ كان يأمرنا أن نخرج الصدقة من الذي نعد للبيع»

**"Zaidi ya hivyo ni kwamba Mtume SAW ame tuamrisha kutoa sadaqa kwa kile tulicho uza"**

Uwajibu wa Zakat kwa biashara ulielezewa kutoka kwa Umar ra pia na mwanaye, na Ibn Abbas, na wanazuoni saba wa fiqh pamoja nawo ni Hassan, Jabbir, Tawoos, al-Nakha'i, a-Thawri, al-Awzaa'i, a-Shafi'i, Ahmad, Abu Obeid, na Abu Hanifa, and wengine.

Biashara inawajibikiwa na Zakat iwapo itafikia kipimo cha kisheria, yaani **Nisab ya Dhahab** au **Nisab ya fedha (silver)** ikipitikiwa na mwaka mmoja.

Iwapo mfanyabiashara ameanza na biashara yake kwa mtaji ambao hauja fikia kiwango cha **Nisab** na mwishoni mwa mwaka mtaji wake umekuwa na kufikia **Nisab** haimlazimu kutoa Zakat kwa sababu hiyo **Nisab** haija zungukiwa na mwaka. Atawajibika kulipa Zakat baada ya kiasi hiki cha fedha kupitikiwa na mwaka (al-Hawl)

Na ikiwa mfanyabiashara ameanza biashara yake kwa mtaji ambao unafikia kiwango cha **Nisab,** kwa mfano labda ameanza kwa mtaji wa Dinar 1,000, mwishoni mwa mwaka ikawa biashara yake imekua na kupata kipato, akawa sasa ana Dinar labda 3000, basi anawajibika kulipa Zakat kwa zile Dinar 3,000 na wala sio kwa Dinar 1,000 aliyo anzia biashara, na wala haitakuwa Zakat kwa faida tu aliyo kusanya kupitia mtaji huo, bali analazimika kulipa Zakat kwa fedha jumla aliyo imiliki, yaani Dinar 3,000. Sababu yakufanya hivi ni kwamba faida iliyo patikana na kukua kwa bisahara imo ndani ya fedha hizi, Dinar 3000, na muda ulio fikia faida hii ndiwo pamoja na mtaji.

Kwa sura nyingine jambo hili liko hivi:

1. Iwapo thamani ya bidhaa imefikia **Nisab,** ambayo imefikia Dinar 20 za Dhahab, yaani gram 85 za Dhahabu, au Dirham 200 za fedha (silver) ambayo ni gram 595 za fedha (silver)… basi inarekodiwa tarehe hii ilipofikia **Nisab** na inakuwa ndiyo pa kuanzia kuhesabu mwanzo wa mwaka, mwaka wa Hijria.

2. Mwishoni mwa mwaka (al-Hawl) ina kokotolewa thamani ya mali aliyokuwa nayo, (mtaji pamoja na faida) na kisha atatoa Zakat kwa kiwango cha 1/40 (sawa na 2.5%).

3. Baada ya maelezo haya, jawabu kwa swali lako nikama ifuatavyo:

a. Kwa mwaka uliyopita ulikuwa na mtaji wa Dola 100,000 kwa ajili ya kufanyia biashara, kiasi hiki ni zaidi ya **Nisab.**

b. Kutokana na biashara yako katika mchakato wa kununua na kuuza majumba umepata faida ya Dola 20,000 kwa mwaka.

c. Mwishoni mwa mwaka, "al-Hawl", umekuwa na jumla ya Dola 120,000.

d. Zakat kwa msingi huu ina lipwa kutoka pesa yote ya biashara yako hii, yaani pesa kamili uliyo nayo na wala sio tu kwa pesa ya faida. Kwahiyo Zakat yako ni kutoka Dola 120,000 ambayo ni 2.5% sawa na Dola 3,000.

**Ndugu yako,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**



# SAUDIA: CHAGUO LA KWANZA LA TRUMP

Trump atua Saudia tarehe 21 May 2017 kwa ziara ya kuweka mbinu mpya ya kuwagawa waislamu ulimwenguni ili Marekani iweze kutekeleza vizuri sera yake ya nje ya ugaidi na uislamu wa siasa kali. Pia katika ziara hiyo Marekani itafanya biashara kubwa ya silaha ya mabilioni ya dola na kuipa tahfif ya uchumi wake na kuufunika macho ulimwengu wa kiislam kuwa waislamu watanufaika na ziara hiyo. https://www.washingtonpost.com/politics/trump-gets-elaborate-welcome-in-saudi-arabia-embarking-on-first

Wakati wa utawala wa Obama ,aliichaguwa Misri kimkakati wa kujifanya hana nia mbaya na uislamu mwaka 2009 mjini Cairo kwa kuanza na Assalaam alakum na kuitikuza kiuongo Qurani kuwa ni kitabu kitakafu katika hotuba yake ya dakika 55. Baadae akaweka mkakati wa kuunga mkono Shia na kuhakikisha watawala mfano Iraq wanakuwa mashia tu kuanzia Iyad Alawi hadi Nour Al Malik tokea Marekani kuikalia rasmi Iraq mwaka 2003 kwa mlango wa nyuma baada ya vita vya Ghuba vya 1991 hali ambayo imesababisha mamilioni ya waislamu kuuwana wenyewe kwa wenyewe na kuzaa chuki mtawaliya.obamawhitehouse.archives.gov/blog/2009/06/04/

Marekani imegeuza mbinu yake ya kuugawa ulimwengu wa kiislamu na kukuza ugomvi wa kimadhehebu na kuchagua sunni badala ya shia, yaani ni kinywaji kile kile ndani ya chupa nyengine .Trump amegeuza mbinu hiyo hiyo kwa kuunga mkono Sunni dhidi ya Shia kwa lengo hilo hilo la Obama kwa kuwashutumu Iran kuunga mkono makundi yenye kuleta ugomvi katika jamii .Pia aliisifu Saudia kuwa ni ardhi takatifu na haipaswi kukaliwa na magaidi na laiki yao ni kufurushwa ardhi zote za Mashariki ya kati. Katika hotuba yake aliiwashia moto Iran kuwa ni inachochea migogoro ya makundi katika jamii na ilhali nayo ni kibaraka wake.

www.christianpost.com/news/president-trump-condemns

Kwanini Trump achague Saudia katika ziara yake hii ya mwanzo Mashariki ni suala linahitaji kutafakari vya kutosha :-

Sababu kubwa nafasi iliyojipachika Saudia ya kuwa kiongozi wa misikiti mitukufu ya Makka na Madina .Kijografia misikiti hiyo imo ndani ya Saudia na Waislamu kiuhalisia wanaichukuliwa kiitikadi misikiti hiyo miongoni mwa mambo matukufu kwao (shaairi).Hivyo ushawishi wake kwa waislamu wengi ulimwenguni ni mkubwa.

Sababu ya pili ni Saudia kutumia utajiri wake kusaidia na kugharamia nafasi nyingi za masomo, kujenga misikiti ya kifahari na hata kugawa misahafu bure na kukuza madhehebu ya Answar sunna . Kutokana na sababu hizo na nyenginezo Saudia inaonekana na waislamu wengi kuwa ni kioo kwao .Makundi ya madhehebu ya Answar sunna baadhi yao hutumiwa na Saudia kutekeleza sera na ajenda zake nje ya mipaka ya nchi yake kama lilivyotumika kundi la mujahedeen kumuondoa Dr Najibullah na marafiki zake wa Urusi huko Afghanistan mwaka 1992 kwa maslahi ya Marekani . https://en.wikipedia.org/wiki/Mohammad_Najibullah .na hivi sasa mujahedeen wa aina hiyo hiyo wanatumika Syria . en.wikipedia.org/wiki/Mujahideen

Sababu ya tatu ni kwa Saudia kujitolea kwa hali na mali kuunga mkono sera ya Marekani na UN ya kupambana na ugaidi na uislamu wa siasa kali. Mwaka 2004 Saudia ilitoa kitita cha Dola $ 100 kuipa UN kuchangia sera hiyo ya ugaidi ifanikiwe ulimwenguni.Kwa hivyo Saudia ni mshirika mwanifu wa kuangamiza uislamu na waislamu. www.nytimes.com/2014/08/14/world/middleeast/

Sababu ya nne ni kukuza ushirikiano baina ya Marekani na Saudia ambao ulitiwa saini na Raisi Roosevelt na Mfalme mwaka 1931.

Enyi watukufu waislamu, bado tuna shaka na mwenendo mzima wa Ufalme wa Saudia kuwa una uadui bayana kwa Uislamu na Waislamu? Kinachofanyika ni kujificha gongo nje kwetu. Lakini Allah katuwekea wazi sura halisi ya watawala wanao simamia misikiti mitukufu Makka na Madina.Allah anatupa ahadi na bishara ya kushindwa njama za makafiri na wanaoshirikiana nao:-

**إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ لِيَصُدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ فَسَيُنفِقُونَهَا ثُمَّ تَكُونُ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُونَ وَالَّذِينَ كَفَرُوا إِلَى جَهَنَّمَ يُحْشَرُونَ**

*“Hakika ya wale walio kufuruhutoa mali zao ili kuzuilia njia ya Allah SWT.Basi watazitoa hizo malikisha zitakuwa majuto yao, kasha watashindwa. Na wale waliodumu katika ukafiri watakusanywa katika Jahannamu”.(8:36)*

Tumepewa na Allah dalili wazi kuwa kwa hakika daima Makafiri na washirika wao watakusanya nguvu zao za hali na mali kuupiga vita uislamu na waislamu kama inavyofanya Saudia kushirikiana na Marekani.Lakini Allah ametupa bishara pia kuwa mwisho watashindwa .Kwa hivyo kilichobaki kwetu waislamu sote tuliokubali kumpwekesha na kumtegemea Allah SWT ni kufanya juhudi kuirejesha dola ya kiislam/khilafah chini ya usimamizi wa Khalifah kama alivyotuelekeza Mtume saaw iwakomboe waislamu dhidi ya watawala wenye kutekeleza ukafiri wazi wazi kama Saudia na wengineo.

**Na Suleiman Mbarouk-Ticha Sule**



**RAMADHANI NA UZINDUZI WA CHANNELI YA TV, WAQIYAH TV, YA HARAKATI YA HIZB UT-TAHRIR ULIMWENGUNI**



**WANAHARAKATI WA HIZB UT-TAHRIR WAKIWA KATIKA JUKUMU LA KUWAFIKISHIA WAISLAM UFAHAMU NA DHAQAFA SAHIHI YA KIISLAM KWA NJIA YA VITABU NA CD NJE YA MASIJID LUUTA KIEMBE SAMAKI ZANZIBAR KUNAKO FANYIKA MASHINDANO YA KUHIFADHI QUR'AN Ramadhani 1438H**



**TEMBELEA**

**UKURASA WA FACEBOOK WA AMIRI WA HIZB UT-TAHRIR**

***Kujiongezea mwamko wa usul ul- fiqhi, siyasa, uchambuzi nk.***

**www.facebook.com/AmeerhtAtabinKhalil**